



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA  
WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU CHETI DARAJA LA A  
(GATCE) 2020**

**634 STADI ZA KAZI**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA  
WATAHINIWA WA UALIMU CHETI DARAJA LA III A  
(GATCE) 2020**

**634 STADI ZA KAZI**

*Kimechapishwa na:*  
Baraza la Mitihani la Tanzania,  
S.L.P 2624,  
Dar es salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020

Haki zote zimehifadhiwa.

## **YALIYOMO**

|  |    |
|--|----|
| DIBAJI.....  | iv |
| 1.0 UTANGULIZI.....  | 1  |
| 2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI .....            | 2  |
| 2.1 SEHEMU A: (Taaluma na Utaalamu) .....                            | 2  |
| 2.2.1 Swali la 1: Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo.....     | 2  |
| 2.2.2 Swali la 2: Upigaji wa Picha.....                              | 5  |
| 2.2.3 Swali la 3: Muziki.....  | 7  |
| 2.2.4 Swali la 4: Ufundishaji .....                                  | 9  |
| 2.2.5 Swali la 5: Misingi ya Kufundishia Somo la Stadi za Kazi.....  | 10 |
| 2.2.6 Swali la 6: Ushoni wa Nguo .....                               | 11 |
| 2.2.7 Swali la 7: Kilimo, Ufugaji na Uvuvi .....                     | 13 |
| 2.2.8 Swali la 8: Ufundishaji .....                                  | 15 |
| 2.2.9 Swali la 9: Upigaji Picha .....                                | 17 |
| 2.2.10 Swali la 10: Ufundishaji .....                                | 20 |
| 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma).....                        | 22 |
| 2.2.1 Swali la 11: Ufundji Viatu .....                               | 22 |
| 2.2.2 Swali la 12: Ususi .....                                       | 26 |
| 2.2.3 Swali la 13: Ushoni wa Nguo .....                              | 29 |
| 2.3 SEHEMU C: Maswali ya Insha (Utaalamu) .....                      | 33 |
| 2.3.1 Swali la 14: Misingi ya Kufundishia Somo la Stadi za Kazi..... | 33 |
| 2.3.2 Swali la 15: Upimaji .....                                     | 36 |
| 2.3.3 Swali la 16: Sanaa za Maonyesho .....                          | 42 |
| 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA<br>MADA .....         | 47 |
| 4.0 HITIMISHO .....  | 47 |
| 5.0 MAPENDEKEZO .....  | 48 |
| <i>Kiambatisho</i> .....   | 49 |

## **DIBAJI**

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitimu Mafunzo ya Ualimu Daraja la III A kwa somo la Stadi za Kazi. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa wanachuo, wakufunzi, waandaa sera, wadau wa elimu na jamii kwa ujumla jinsi watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani.

Taarifa hii ni tathmini ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi. Kimsingi, majibu ya watahiniwa katika maswali ya mtihani ni uthibitisho wa yale ambayo mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa katika mafunzo ya Ualimu katika daraja hili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vizuri au vibaya katika kujibu maswali ya mtihani. Sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kushindwa kupata alama za juu katika baadhi ya maswali ni pamoja na kushindwa kuelewa matakwa ya maswali, kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana zilizopimwa, kutoa maelezo yasiyojitosheleza na uelewa mdogo katika kujibu maswali ya insha. Baraza la Mitihani la Tanzania linaamini kuwa mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wakuu wa vyuo, wathibiti ubora wa elimu, wakufunzi na wanachuo kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, Watahini wa somo na wadau wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kutayarisha taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde  
**KATIBU MTENDAJI**

## **1.0 UTANGULIZI**

Mtihani wa somo la Stadi za Kazi kwa watahiniwa wa mtihani wa Ualimu Daraja la IIIA uliofanyika Julai 2020 uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Stadi za Kazi wa mwaka 2009 na fomati ya mtihani ya mwaka 2017.

Mtihani huu ulikuwa na jumla ya maswali kumi na sita (16) yaliyogawanywa katika sehemu tatu: A, B na C. Sehemu A ilikuwa na maswali 10 ya majibu mafupi kutoka katika mada za taaluma na ufundishaji. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote. Sehemu B ilikuwa na maswali matatu ya insha kutoka katika mada za taaluma ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili. Aidha, sehemu C ilikuwa na maswali matatu ya insha kutoka katika mada za ufundishaji na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili. Mtihani wote ulikuwa na alama 100 zilizogawanywa katika sehemu A, B na C. Sehemu A ilikuwa na jumla ya alama 40 na kila swali lilikuwa na alama 4, wakati sehemu B na C zilikuwa na jumla ya alama 30 kila moja na kila swali lilikuwa na alama 15.

Ufaulu wa watahiniwa katika mtihani wa somo la Stadi za Kazi kwa mwaka 2020 ulikuwa mzuri. Jumla ya watahiniwa 3,313 walifanya mtihani, kati yao watahiniwa 3,296 sawa na asilimia 99.49 walifaalu kwa kupata alama 40 na zaidi. Aidha, watahiniwa 17 sawa na asilimia 0.51 walifeli kwa kupata gredi F. Kiwango cha ufaulu kwa mwaka 2020 kimepungua kwa asilimia 0.49 ikilinganishwa na mwaka 2019 ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 99.98. Kati ya watahiniwa wote waliofanya mtihani asilimia 0 walipata daraja A, asilimia 6.52 walipata daraja B, asilimia 69.88 walipata daraja C, asilimia 23.09 walipata daraja D na asilimia 0.51 walipata daraja F. Ufaulu wa watahiniwa umegawanyika katika viwango vitatu ambavyo ni kizuri, wastani na hafifu. Ufaulu mzuri unaanzia alama 70 hadi 100, wa wastani unaanzia alama 40 hadi 69 na hafifu unaanzia alama 0 hadi 39.

Chati za viwango vya ufaulu kwa asilimia zimeambatanishwa ili kufafanua ufaulu wa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, rangi ya njano ufaulu wa wastani na rangi nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.

Taarifa hii inachambua maswali yenyeye ufaulu mzuri, wastani na hafifu ili kuongeza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi

za Kazi. Aidha, taarifa hii pia inaonesha sababu zilizowafanya watahiniwa kupata ufaulu mzuri, wastani au hafifu katika majibu ya maswali ya baadhi ya mada. Sampuli za majibu ya watahiniwa zimeambatanishwa ili kuonesha kile walichofanya. Hivyo, uchambuzi huu utasaidia kuimarishe ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi kwa mada ambazo ufaulu ulikuwa hafifu ili kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mitihani yao. Aidha, inategemewa kuwa matokeo ya uchambuzi huu yatawanufaisha wanachuo, wakufunzi, waandaaji wa sera na wadau wote wa elimu kwa ujumla.


## **2.0 TATHMINI YA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI**

### **2.1 SEHEMU A: (Taaluma na Utaalamu)**

Sehemu A ilikuwa na maswali ya majibu mafupi yapatayo kumi kutoka katika mada za taaluma na utaalamu. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na jumla ya alama 4. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu, ambapo kiwango cha ufaulu mzuri kilianzia alama 3 hadi 4, ufaulu wa wastani ulianzia alama 2 hadi 2.5 na ufaulu hafifu ulianzia alama 0 hadi 1.5.

#### **2.2.1 Swali la 1: Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo**

Swali hili lilikuwa na vipengele viwili yaani (a) na (b). Kipengele (a) kiliwataka watahiniwa kueleza kwa kifupi maana ya kimia na kipengele (b) kiliwataka watahiniwa kutaja vifaa sita (6) vinavyotumika katika kuchapa kwa njia ya kimia. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa kati ya watahiniwa wote 3,360 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 975 (29.0%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 846 (25.2%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 1,539 (45.8%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5 kama inavyoonekana katika Chati Na. 1.



**Chati Na.1:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa (45.8%) waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, baadhi yao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha juu ya dhana nzima ya uchapaji wa picha kwa njia ya kimia, hivyo kutoa majibu sahihi na yasiyo sahihi. Wengine walidhihirisha kutoelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa majibu yasiyo kuwa na uhusiano na swali. Mfano, mtahiniwa alieleza maana ya kimia kama; *ni chombo cha kieletroniki kinachotumika kuchapa picha mbalimbali*. Aidha, mtahiniwa mwengine alieleza kuwa: *Kimia ni kifaa cha umeme kinachotumika katika kuchapa mfano vitabu badala ya kueleza kwa usahihi maana ya kimia*. Pia katika kipengele (b) alitaja vifaa kama: *Printa, Kompyuta, Kisu, Sindano ya mkono, Cherehani, Kibana kibao, Uzi, Subana*. Aidha, mtahiniwa mwengine alitoa majibu yasiyo sahihi kama: *Apecha, Lenzi, Mboni, Shata, Betri, Kihisi Mwanga* ambavyo vyote ni vifaa vilivyomo katika kamera. Kielelezo Na.1.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

|       |   |
|-------|---|
| 01@   | Maana ya kimia.<br>Ni chombo cha kietoni ki kinachotumia<br>kuchapa picha mbalimbali. |
| (b)   | Vifaa sita vinavyotumika kateka kuchapa<br>kwa njia ya kimia.                         |
| (i)   | Ienzi.  |
| (ii)  | Mbaoni.   |
| (iii) | Shata.  |
| (iv)  | Daiiframu.  |
| (v)   | Betri.  |
| (vi)  | Irissi.   |

Kielelezo Na.1.1: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1

Katika Kielelezo 1.1 mtahiniwa alishindwa kueleza maana sahihi ya kimia na katika kipengele (b) alitaja sehemu za kamera badala ya kutaja vifaa vinavyotumika katika kuchapa kwa njia ya kimia.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa (29.0%) waliopata ufaulu mzuri katika swali hili, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Usanii Wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo*, hususan katika kipengele cha *uchapaji wa picha kwa njia ya kimia*. Watahiniwa hao walielewa matakwa ya swali, hivyo walieleza kwa usahihi maana ya kimia katika kipengele (a) kama; *kimia ni wavu au kitambaa cha hariri ambacho huwambwa kwenye fremu ya mbao au plastiki na kufanana na chekecheke la unga*. Vilevile katika kipengele (b) waliweza kutaja vifaa sita vinavyotumika katika kuchapa kwa njia ya kimia kama; *fremu ya mbao, magazeti, karatasi, gundi ya utepe, stenseli na rangi*. Kielelezo Na.1.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyweweza kujibu swali hili kwa usahihi.

|    |  |
|----|--|
| 1. | (a) <i>Kimia</i><br>Ni kifaa ambacho kinetengenezwa<br>kwa mbao na kufarania na cheke<br>cheo la unga kwa kuekewa nyaru<br>Chini                       |
|    | (b) (i) <i>Magereti'</i><br>(ii) <i>Kifaaibaa</i><br>(iii) <i>Stenzel'</i><br>(iv) <i>Finia</i><br>(v) <i>Kisambazio cha rangi</i><br>(vi) <i>Piza</i> |


Kielelezo Na.1.2: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1

Katika Kielelezo Na.1.2 mtahiniwa aliweza kueleza kwa usahihi maana ya kimia na pia aliweza kutaja vifaa sita vinavyotumika katika kuchapa kwa njia ya kimia hivyo alipata ufaulu mzuri.

Aidha, watahiniwa (25.2%) waliopata ufaulu wa wastani katika swali hili, walionesha kuwa na maarifa ya wastani kuhusu dhana ya *uchapaji kwa njia ya kimia*. Baadhi ya watahiniwa hao walitoa hoja pungufu na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alirudia hoja kama vile: *mbao ya kimia, fremu ya kimia*, hivyo kupata alama za wastani.

## 2.2.2 Swali la 2: Upigaji wa Picha

Swali hili liliwataka watahiniwa kutaja kanuni nne za upigaji wa picha tuli zinazotakiwa kupitiwa na mwalimu kabla ya kuanza kufundisha mada hiyo darasani. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa, kati ya watahiniwa wote 3,360 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 273 (8.0%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 361 (10.5%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2,726 (81.5%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, swali hili likiwa na ufaulu hafifu kwa kuwa ni asilimia 18.5 pekee ya watahiniwa ndio walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.2.



**Chati Na.2:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ulionesha kuwa, watahiniwa (81.5%) waliopata ufaulu hafifu, baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana husika na hivyo kutoa hoja pungufu na wengine kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Watahiniwa wengine (54.2%) waliopata alama 0 katika swali hili, hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo walitoa hoja zisizohusiana na swali. Mfano, mtahiniwa alitaja kanuni za kupiga picha kama: *ubunifu, usimamaji, uoni, mizani, kuvaan mkanda wa kamera na kufungua kamera*. Mtahiniwa mwengine katika kundi hili aliandika hoja kama; *kaza miguu, kushirikisha wanafunzi katika matumizi ya vifaa na awe na aina mbalimbali za picha tuli*. Kielelezo Na.2.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

|   |                             |
|---|-----------------------------|
| 2 | i) Lazima ziwe qsimidhuruwa |
|   | ii) Lazima zinapakwe rangi  |
|   | iii) Lazima ziwe nadhiifu   |
|   | iv) Lazima ziwe na yfumbi   |

**Kielelezo Na.2.1:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2

Katika Kielelezo Na.2.1 mtahiniwa alitaja sifa za picha tuli badala ya kutaja kanuni nne za upigaji wa picha tuli zinazotakiwa kupitiwa na mwalimu kabla ya kwenda kufundisha darasani

Aidha, watahiniwa (8.0%) waliopata ufaulu mzuri katika swali hili, walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Upigaji Picha*. Watahiniwa hao waliweza kutaja kanuni zisizopungua tatu za upigaji picha tuli zinazotakiwa kupitiwa na mwalimu kabla ya kwenda kufundisha darasani kama: *kuwepo kwa mwanga wa kutosha, kuwepo kwa vifaa na vitu vinavyopigwa picha, kuwepo kwa umbali kati ya kitu kinachopigwa picha na kamera na kuwepo kwa utulivu wakati wa kupiga picha*. Kielelezo Na.2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa alijejibu swali hili kwa usahihi.


|    |  |
|----|--|
| Q. | <p>a) kuwepo kwa mwanga wa kutosha.</p> <p>b) kuwepo kwa vifaa vinavyotumika kupiga picha</p> <p>c) kuwepo kwa kitu kinachopigwa picha</p> <p>d) Umbali kati ya kitu kinachopigwa picha na kamera.</p> |
|----|--|

Kielelezo Na.2.2: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2

Katika Kielelezo Na.2.2 mtahiniwa alitaja kanuni nne za upigaji wa picha tuli zinazotakiwa kupitiwa na mwalimu kabla ya kwenda kufundisha darasani, hivyo alipata ufaulu mzuri.

### 2.2.3 Swali la 3: Muziki

Swali hili liliwataka watahiniwa kuonesha kwa hoja nne faida za muziki katika jamii. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa, kati ya watahiniwa wote 3,360 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 3,316 (98.7%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 6 (0.2%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 38 (1.1%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 98.9 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na. 3.



**Chati Na.3:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa (98.7%) waliopata ufaulu mzuri walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya Muziki. Watahiniwa hao waliweza kuonesha faida za muziki katika jamii kama: *kuburudisha jamii, kuelimisha jamii, kuonya jamii, kuongeza pato la taifa na kuto ajira*. Hii inadhihirisha watahiniwa hao walielewa vyema matakwa ya swali na hivyo walipata alama za juu. Kielelezo Na.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

|    |   |
|----|---|
| 8. | <i>1) Kuburudisha jamii</i><br><i>2) Kuelimisha jamii</i><br><i>3) Chanzo cha ajira</i><br><i>4) Kuborsoa na kuonya jamii</i> |
|----|---|

Kielelezo Na.3: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3

Katika Kielelezo Na.3 mtahiniwa aliweza kutaja faida za muziki katika jamii na hivyo kupata ufaulu mzuri.

Kwa upande mwingine watahiniwa wachache (1.1%) waliopata kiwango hafifu cha ufaulu baadhi yao walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana ya Muziki hivyo kutoa hoja pungufu au kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Wengine

waliopata alama 0 hawakuelewa matakwa ya swali na hivyo kutoa majibu tofauti na kilichoulikizwa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama; *kujua kuchenza muziki, hutoa maumivu na huleta mabadiliko.*

#### 2.2.4 Swali la 4: Ufundishaji

Swali hili liliwataka watahiniwa kueleza kwa kifupi aina nne za majadiliano zinazoweza kutumika kufundisha mada ya Ususi. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa, kati ya watahiniwa wote 3,360 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 293 (8.7%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 670 (20.0%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 2,396 (71.3%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa ni asilimia 28.7 pekee ya watahiniwa ndio walipata kuanzia alama 2 hadi 4.

Watahiniwa (71.3%) waliopata alama hafifu, asilimia 46.6 walipata alama 0. Watahiniwa hawa baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizo sahihi kama vile: *mwanafunzi na zana za ususi, vifaa vyaa ususi na mwalimu, mwalimu kuchagua makundi ya kazi, mwalimu kugawa makundi ya wanafunzi.* Watahiniwa wengine hawakuwa na uelewa kuhusu mada ya ufundishaji hususan aina za mbinu za majadiliano, hivyo walitoa majibu yasiyohusiana na matakwa ya swali. Mfano mtahiniwa mmoja aliandika majibu kama: *majadiliano ya kitaalamu, majadiliano ya vitendo, majadiliano ya nadharia na majadiliano ya onesho mbinu.* Kielelezo Na.4 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

|    |  |
|----|--|
| 1p | a) oneshombini<br>b) Majadiliano ya vikundi<br>c) Changanya kete.<br>d) Matembezi ya galale. |
|----|--|


Kielelezo Na.4: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 4

Katika Kielelezo Na.4 mtahiniwa alitaja mbinu za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi badala ya kueleza kwa kifupi aina nne za majadiliano zinazoweza kutumika kufundishia mada ya Ususi.

Uchambuzi zaidi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa wachache (8.7%) waliopata ufaulu mzuri katika swalii hili walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya mbinu za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi. Watahiniwa hao waliweza kueleza aina nne za majadiliano zinazoweza kutumika katika kufundishia mada ya Ususi kama: *makundi madogo, jozi ya watu wawili, muhadhara na jopo*. Watahiniwa hawa walielewa vyema matakwa ya swalii. Sababu nyingine iliyosababisha kutoa majibu sahihi ni kuwa, mada ya mbinu za kufundishia na kujifunzia pia hufundishwa katika masomo mengine hususan Ualimu, hivyo waliweza kuhawilisha maarifa.

#### 2.2.5 Swali la 5: Misingi ya Kufundishia Somo la Stadi za Kazi

Swali hili liliwataka watahiniwa kuainisha hatua nne za kufuata katika kuhakikisha usafi na usalama wa chakula jikoni. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa, kati ya watahiniwa 3,360 (100%) waliofanya swalii hili, watahiniwa 3,359 (76.7%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 329 (9.8%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 324 (13.6%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, swalii hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 86.5 ya watahiniwa walipata alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.4.



Chati Na.4: Ufaulu wa watahiniwa katika swalii la 5

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa watahiniwa (76.7%) waliopata ufaulu mzuri walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya Misingi ya Kufundishia somo la Stadi za Kazi. Watahiniwa hao waliweza kuainisha hatua nne za kufuata katika kuhakikisha usafi na usalama wa chakula jikoni. Mfano wa baadhi ya majibu sahihi yaliyoainishwa ni: *kusafisha chumba cha jiko mara kwa mara, kufunga kitambaa puan na kichwani kama una nywele ndefu ili kuzuia zisingie kwenye chakula, hakikisha unaosha vyakula kabla ya kupika, kuhakikisha unakata kucha ndefu na kunawa mikono ili kuondoa uchafu na kuhakikisha unaosha matunda kabla ya kula.* Kielelezo Na.5 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

|      |  |
|------|--|
| s    | i) funika kichwa kwa kitambaa au kopja<br>ikiwa una nywele ndefu.                      |
| ii)  | Hukata kuchoa ndefu wakati unapokuwa jikoni ili kuepusha uchafu kuingia kwenye chakula |
| iii) | Kunawa mikono kwa sabuni na maji safi kabla ya kuanza kupika                           |
| iv)  | Vyakula vyaote vijunikiwe  |


Kielelezo Na.5: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa watahiniwa (13.6%) waliopata ufaulu hafifu baadhi yao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana husika hivyo walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Wengine hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliainisha hatua nne za kufuata kama: *kukipanga kwa utaratibu, kuzuia wanyama kuingia na kufunga jiko kwa usalama, zilizosababisha kupata alama haffifu.*

## 2.2.6 Swali la 6: Ushoni wa Nguo

Swali hili liliwataka watahiniwa kuorodhesha vifaa nane vitakavyowasaidia kuwawezesha wanafunzi wao kupata stadi ya utarizi. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa, watahiniwa wote 3,360 (100%) walifanya swali hili, ambapo watahiniwa 1,746 (52%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 1,290 (38.4%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5. Vilevile watahiniwa 324

(9.6%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa asilimia 90.4 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.5.



**Chati Na 5:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6*

Watahiniwa (52%) waliopata ufaulu mzuri walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Ushoni wa Nguo*. Watahiniwa hao waliweza kuorodhesha vifaa nane vitakavyosaidia kuwawezesha wanafunzi kupata stadi ya utarizi kama vile: *nyuzi za rangi, sindano ya mkono, kibanio cha kitambaa, pete ya kutarizi, subana ya kuvalaa katika kidole, michoro ya mapambo, penseli na karatasi ya kaboni*. Sababu zilizopelekea watahiniwa kufanya vizuri swali hili ni kuwa somo hili hufundishwa kwa vitendo zaidi na watahiniwa huweza kujenga kumbukumbu ya kutosha kuhusu dhana husika na vifaa vinavyotumika. Kielelezo Na.6.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

|    |   |
|----|---|
| 6. | <ul style="list-style-type: none"> <li>i&gt; Uzi wa rangi mbalimbali</li> <li>ii&gt; Subana ya mkononi</li> <li>iii&gt; Kitambaa</li> <li>iv&gt; Cherehani ya kufanizia</li> <li>v&gt; Sindano ya kushonea</li> <li>vi&gt; Mapambo mbalimbali</li> <li>vii&gt; Kipimo</li> <li>viii&gt; Penseli / chaki kwa ajili ya kuweka alama.</li> </ul> |
|----|---|

Kielelezo Na.6.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6

Katika Kielelezo Na.6.1 mtahiniwa aliweza kuorodhesha vifaa nane vitakavyosaidia kuwawezesha wanafunzi kupata stadi ya utarizi, hivyo kupata ufaulu mzuri.

Kwa upande mwingine asilimia 9.6 ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, baadhi yao hawakuwa na maarifa kuhusu dhana ya utarizi hivyo kutoa majibu dhaifu. Wengine hawakuelewa matakwa ya swali hivyo walitoa majibu yasiyohusiana na swali. Mfano mtahiniwa mmoja aliandika; *kofia, meza na kitu*. Mtahiniwa mwengine aliandika; *kitabu cha kiada, kitabu cha ziada, ubao wa chaki, mazoezi, mitihani, majaribio, maswali na majorida* kama inavyoonekana katika Kielelezo Na 6.2.

|    |                      |
|----|----------------------|
| 6. | i) Kitabu cha kiada  |
|    | ii) Kitabu cha ziada |
|    | iii) Majanipa        |
|    | iv) Ubao wa chaki    |
|    | v) Mazoezi           |
|    | vi) Majaribio        |
|    | vii) Mitihani        |
|    | viii) maswali        |


Kielelezo Na.6.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 6

Katika Kielelezo Na.6.2 mtahiniwa aliorodhesha vifaa vya mtaala na zana za upimaji badala ya vifaa vitakavyomsaidia mwalimu kuwawezesha wanafunzi kupata stadi ya utarizi, hivyo kupata alama 0.

## 2.2.7 Swali la 7: Kilimo, Ufugaji na Uvuvi

Swali hili liliwataka watahiniwa kubainisha njia nne za kudumisha afya njema ya wanyama wanaofugwa. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa, kati ya watahiniwa wote 3,360 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 3,284 (97.7%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 34 (1.0%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 42 (1.3%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa

asilimia 98.7 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.6.



**Chati Na.6:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa (97.7%) waliopata ufaulu mzuri walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Kilimo, Ufugaji na Uvuvi*. Watahiniwa hao waliweza kubainisha njia tatu hadi nne za kudumisha afya njema ya wanyama wanaofugwa. Mfano wa majibu sahihi ya watahiniwa ni kama: *kuwatibu wanyama wanapougua, kuwapa wanyama dawa za chanjo dhidi ya magonjwa, kuzingatia usafi wa nje na ndani ya banda la wanyama, kutofuga wanya wengi katika eneo moja na kuzingatia usafi wa vyombo vya chakula na maji*. Sababu nyengine iliyopelekea watahiniwa kufaulu vizuri swali hili ni kwamba waliweza kuhusianisha maarifa waliyopata darasani na shughuli za ufugaji zinazofanyika katika jamii wanamoishi. Kielelezo Na.7 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

|    |   |
|----|---|
| 7. | i) Kuwapa wanyama chakula bora  |
|    | ii) Kuwapo wanyama chanjo za magonjwa<br>mbalimbali mara kwa mara             |
|    | iii) Kufuga wanyama katika banda zuri na safi<br>ambalo linapikisha hewa safi |
|    | iv) Kuwapa wanyama maji safi  |

Kielelezo Na.7: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 7

Katika Kielelezo Na.7 mtahiniwa aliweza kubainisha njia nne za kudumisha afya njema ya wanyama wanaofugwa na hivyo alipata alama za juu.

Kwa upande mwingine asilimia 1.3 ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu katika swali hili, wengi walikuwa na mapungufu katika majibu yao kama; kutoa hoja pungufu na kuchanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Wengine hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa majibu yasiyoendana na matakwa ya swali. Mfano mtahiniwa mmoja alibainisha njia hizo kama; *kuleta afya katika jamii, kutegeneza nguo na ngoma, kutumika kwa nyama na kuongeza kipato*. Mtahiniwa alitaja faida za kufuga wanyama badala ya njia za kudumisha afya njema ya wanyama wanaofugwa, hivyo alipata alama 0.

### 2.2.8 Swali la 8: Ufundishaji

Swali hili liliwataka watahiniwa kuonesha udhaifu wa mbinu ya kushirikisha kidogo katika ufundishaji wa mada ya *udobi*, kwa hoja nne. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa, kati ya watahiniwa wote 3,360 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 2,946 (87.7%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4. Watahiniwa 173 (5.1%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 241 (7.2%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 92.8 ya watahiniwa waliweza kupata kuanzia alama 2 hadi 4.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa (87.7%) waliopata ufaulu mzuri walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mbinu bora za kufundishia mada ya ufundishaji. Watahiniwa hao waliweza kuonesha kwa hoja nne udhaifu wa mbinu ya kushirikisha kidogo katika ufundishaji wa mada ya *udobi*. Mfano wa majibu sahihi ya watahiniwa ni kama: *humchosha mwanafunzi, mwanafunzi kukosa uwezo wa kufikiri kwa kina, hupunguza ari ya mwanafunzi katika kujifunza maarifa ya juu, humfanya mwanafunzi kuwa msikilizaji tu na humnyima mwanafunzi nafasi ya kutoa mawazo kwani humwamini mwalimu zaidi*. Sababu nyingine iliyosababisha kutoa majibu sahihi ni kuwa mada ya ufundishaji hufundishwa katika masomo mengine hususani somo la Ualimu, hivyo kuweza kuhawilisha maarifa. Kielelezo Na.8.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

|  |   |
|--|---|
|  | <p><i>¶ Zifuatayo ni madhaifu ya mbinu ya shififi kushirikisha kidogo katika ufundishaji wa mada ya udobi.</i></p> <ul style="list-style-type: none"> <li>I) Harchachei udadi ya mwanafunzi</li> <li>ii) Hawezi kutoka kwenkweni ya kudumu kwa mwanafunzi</li> <li>iii) Hawezi kutoka ukurasa waenye kwa mwanafunzi</li> <li>IV) Hawezi kutoka Vipaji kwa wanafunzi.</li> </ul> |
|--|---|

Kielelezo Na.8.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 8

Katika Kielelezo Na.8.1 mtahiniwa aliweza kuonesha madhaifu ya mbinu ya kushirikisha kidogo katika ufundishaji wa mada ya udobi na hivyo alipata ufaulu mzuri.

Kwa upande mwingine asilimia 7.2 ya watahiniwa waliopata kiwango hafifu cha kufaulu katika swali hili, baadhi yao walionesha kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mbinu bora za kufundishia mada ya ufundishaji na wengine kushindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa majibu yasiyo sahihi. Mfano mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama; *kujua namna ya kupasi, kutofuata kanuni za ufuaji, kutofuatwa kwa hatua za ufuaji na kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa wayafikie wanafunzi*. Mtahiniwa mwengine aliorodhesha majibu yasiyoendana na

matakwa ya swalii, kama: *siyo rafiki kwa darasa lenye wanafunzi wengi, inatumia gharama kubwa, inatumia muda mwingu wakati wa uandaji wa vifaa na kufanya ufundishaji na ujifunzaji kuwa mgumu kama mwalimu asipoaandaa vizuri.* Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa hizi ni hasara za kutumia mbinu ya ziara kufundishia na siyo udhaifu wa kutumia mbinu ya kushirikisha kidogo kufundishia mada ya *Udobi*. Kielelezo Na. 8.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu vizuri swalii hili.


|    |   |
|----|---|
|    |   |
| 8. | i) Kushidua kufuata taratibu za kupiga pasi nguo.                     |
|    | ii) Kuto kuwa mukini katika kutumia vifaa vya udobi.                  |
|    | iii) Kuto kuwa nadhi fu.  |
|    | iv) Wakati wa kufua kuchanganya nguo zisizorangi na nguo zenye rangi. |
|    |   |
|    |   |

Kielelezo Na.8.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swalii la 8

Katika Kielelezo Na. 8.2 mtahiniwa alieleza kanuni za udobi na kupiga pasi nguo badala ya kuonesha udhaifu wa mbinu ya kushirikisha kidogo katika ufundishaji wa mada ya udobi.

### 2.2.9 Swalii la 9: Upigaji Picha

Swali hili lilikuwa na vipengele viwili; (a) kiliwataka watahiniwa kueleza kwa kifupi njia mbili za utunzaji wa picha na (b) kwa kutoa hoja mbili, kueleza sababu za kutunza picha. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa, kati ya watahiniwa wote 3,360 (100%) waliofanya swalii hili, watahiniwa (77.3%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 608 (18.1%) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 155 (4.6%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swalii hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 95.4 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.7.



**Chati Na.7:** *Ufaulu wa watahiniwa katika swal la 9*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa (77.3%) walipata ufaulu mzuri. Watahiniwa hao walitoa majibu sahihi kwa kipengele (a) kwa kueleza kwa kifupi njia mbili za utunzaji wa picha kwa hoja kama; *kuhifadhi kwenye bahasha, kuhifadhi kwenye albamu, kuhifadhi kwenye fremu ya kioo angavu na kutundika ukutani* na kipengele (b) kwa kutoa sababu za kutunza picha, kama; *zisiharibike, zisichafuke na zisipoteet*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya *Upigaji Picha* na walielewa vyema matakwa ya swal. Kielelezo Na. 9 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swal hili vizuri.

9. Njia za kutunza picha. na sababu za kutunza picha.
- i/ Kwo njia yo album, unawera ulakutunza picha zalcu kwo kuziwelco kwenye albamu yo kutunza picha ili zinwe salamo zaidi.
- ii/ Kwo kuziwelco kwenye bahasho, pio unawera ulakutunza albamu kwo kuziwelco kwenye bahasho ili zisipotee au kuchafule.
- Sababu za kutunza picha.
- iii/ ili zisichafule, pio tunakutunza picha kwenye albamu na bahasho ili zisichafule.
- iv/ ili zisipotee, pio tunakutunza picha ili zisichanike, pio tunakutunza picha ili zisichanike kutoleano na kushilcwo na zolu wengi.
- v/ ili zisijikunje, pio tunakutunza picha kwa kulumio albamu na bahasho ili picha zisijikunje zibala kuwa na mwoneleuno zolle mruu.

Kielelezo Na.9: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 9


Katika Kielelezo Na. 9 mtahiniwa aliweza kueleza kwa kifupi njia mbili za utunzaji wa picha na kutoa sababu mbili za kutunza picha na hivyo kupata alama za juu.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa wachache (4.6%) waliopata ufaulu hafifu, baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine walionesha kutokuwa na maarifa katika mada ya upigaji picha, hivyo walitoa majibu yasiyo sahihi. Mfano wa majibu ya mtahiniwa mmoja yasiyo sahihi ni kama: *kuweka katika matokeo, kuhamasisha jamii, kutunza picha kwa matumizi mbalimbali na kuhifadhi kwenye chumba maalumu cha zana bila*

kujali upande (a) na (b). Mtahiniwa mwingine aliandika hoja kama; *kutunza historia ya jamii* na *kuhifadhi kumbukumbu zetu*, hivyo walipata ufaulu hafifu.

## 2.2.10 Swalii la 10: Ufundishaji

Swali hili liliwataka watahiniwa kutofautisha kati ya ujuzi na lengo mahsus kama vinavyotumika katika Andalio la Somo. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu ulionesha kuwa, kati ya watahiniwa 3,360 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 1,895 (56.5%) walipata kuanzia alama 3 hadi 4, watahiniwa 956 (28.5) walipata kuanzia alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 505 (15.0%) walipata kuanzia alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swalii hili ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 84.9 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 2 hadi 4 kama inavyoonekana katika Chati Na.8.



**Chati Na. 8:** Ufaulu wa watahiniwa katika swalii la 10

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa (50.6%) waliopata ufaulu mzuri walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Ufundishaji*. Watahiniwa hao waliweza kutoa maelezo ya kutosha kutofautisha kati ya ujuzi na malengo mahsus. Mfano wa majibu sahihi ya watahiniwa ni kama vile: *ujuzi ni uwezo wa kutumia maarifa, stadi na mwelekeo anaotakiwa kuupata mwanafunzi, katika kipengele hiki mwanafunzi anatarajiwa kujenga uwezo wa kufikiri na kutenda kupitia mada zilizofundishwa*. Wakati *malengo mahsus ni malengo yanayohusu stadi, mwelekeo na maarifa yanayotarajiwa kufikiwa baada ya mada kukamilika kwa muda maalumu, katika kipengele hiki kinabeba vitendo mbalimbali vinavyosaidia kumjengea mwanafunzi ujuzi na*

*kuweka vigezo vya kumfikirisha ili aweze kutenda.* Watahiniwa hawa walielewa vyema matakwa ya swali. Sababu nyingine iliyosababisha kutoa majibu sahihi ni kuwa, mada hii pia hufundishwa katika masomo mengine kama Ualimu, hivyo waliweza kuhawilisha maarifa. Kielelezo Na.10.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

|     |   |
|-----|---|
|     |   |
| 10. | Tofauti kati ya Ujuzi na Lengo mabsuri ni Ujuzi ni ule uwero wa kufanya kitu au ja mbo fulani baada kufundishwa /kujifunza mada naime katika vipindi kadhaa LAKINI Lengo mabsuri ni matarajio yanayotakiwa kufikiwa na mualimu ndani ya kipindi kim oja na mabadiliko kuonekana kwa mwanafunzi. |
|     |   |
|     |   |
|     |   |

Kielelezo Na.10.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 10

Katika Kielelezo Na.10.1 mtahiniwa aliweza kutofautisha kati ya ujuzi na lengo mabsusi kama vinavyotumika katika Andalio la somo.

Uchambuzi zaidi ulionesha kuwa watahiniwa (28.5%) waliopata ufaulu wa wastani walitoa majibu ambayo hayakukidhi matakwa ya swali. Baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizosahihi na wengine walieleza upande mmoja wa swali.

Pamoja na ufaulu mzuri wa watahiniwa walio wengi katika swali hili watahiniwa wachache (15.0%) waliopata ufaulu hafifu, baadhi yao walikosa maarifa kuhusu mada husika na wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Mfano mtahiniwa mmoja alitofautisha dhana hizo kwa hoja kama: *ujuzi ni malengo ya jumla katika mada ya andalio la somo, na malengo mabsusi ni makusudio kwa mwanafuzi katika kile anachojifunza ambayo si majibu sahihi.* Kielelezo Na.10.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejhindwa kujibu vizuri swali hili.

|    |   |
|----|---|
| 10 | Ujuzi ni jumla ya malengo katika mada<br>lakini<br>malengo mahsus ni uzero wa<br>kufanya kiba katika mada husika<br>katika kujifunza. |
|----|---|

Kielelezo Na.10.2: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 10


Katika Kielelezo Na.10.2 mtahiniwa alishindwa kutofautisha kwa ufasaha kati ya dhana ya ujuzi na lengo mahsus kama vinavyotumika katika Andalio la Somo. Mtahiniwa hakuwa na maarifa kuhusu dhana ya ujuzi na lengo mahsus.

## 2.2 SEHEMU B: Maswali ya Insha (Taaluma)

Sehemu B ilikuwa na maswali ya insha matatu kutoka katika mada za taaluma na mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili tu. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na jumla ya alama 15. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu, ambapo ufaulu mzuri ulianzia alama 10.5 hadi 15, ufaulu wa wastani ulianzia alama 6 hadi 10 na ufaulu hafifu ulianzia alama 0 hadi 5.5.

### 2.2.1 Swali la 11: Ufundı Viatu

Swali hili lilikuwa na vipengele viwili, watahiniwa walitakiwa (a) kufafanua sababu mbili za kufanya matengenezo ya viatu (b) kueleza hatua nne za kufuata katika kukadiria għarama ya vifaa vya kufanyia matengenezo ya viatu. Uchambuzi wa takwimu ulionesha kuwa, watahiniwa 2,855 (84.9%) walijibu swali hili, kati ya watahiniwa 3,360 waliofanya mtihani huu. Watahiniwa 1,112 (38.9%) walipata kuanzia alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 1,567 (54.9%) walipata kuanzia alama 6 hadi 10 na watahiniwa 176 (6.2%) walipata kuanzia alama 0 hadi 5.5. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa ulikuwa mzuri kwa kuwa asilimia 93.8 ya watahiniwa walipata kuanzia alama 6 hadi 15 kama inavyoonekana katika Chati Na.9.



**Chati Na. 9:** Ufaulu wa watahiniwa katika swali la 11

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulionesha kuwa, watahiniwa (38.9%) waliopata ufaulu mzuri katika swali hili waliweza kufafanua kwa ufasaha sababu mbili za kufanya matengenezo ya viatu na kueleza hatua nne za kufuata katika kukadiria gharama ya vifaa vya kufanyia matengenezo ya viatu. Mfano, watahiniwa walifafanua swali hili kwa kutoa majibu sahihi katika kipengele (a) kama; *kuepusha viatu visizidi kuharibika, kumfanya mvaaji apendeze kwa kuwa nadhifu na kupunguza ajali kwa mvaaji;* na kipengele (b) kama; *kubaini vifaa vyote vinavyohitajika, kuandaa orodha ya vifaa vinavyohitajika katika matengenezo ya viatu, kuandika bei ya kila kifaa kinachohitajika katika matengenezo ya viatu kama vile; uzi= tsh 5,000, sindano=tsh 1000, soli=tsh 10,000 n.k,* na *kujumlisha gharama zote za mahaitaji ya vifaa vyote vinavyohitajika vya kutengeneza viatu ili kupata makadirio yote.* Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada nzima ya *Ufund* hususan katika kipengele cha *matengenezo ya viatu.* Kielelezo Na.11 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri na kukidhi matakwa ya swali hili.

11

Materi pengetahuan yang diberikan ini tentang  
 raja wa matu milimpi haribila lava kufanya  
 urekebushaji; ne uboroshaji an ketonganere wa  
 tu nipyap. Materi pengetahuan ya matu buya  
 nyawa lava sababu nipyatara.

Kegushe gharana za kumanne matu  
 nipyap. Utengeneraji wa matu unawereza  
 matu kuskoq gharana katika kumanne  
 matu nipyap.

Kuskoq muda. Utengeneraji wa matu  
 unawereza kuskoq muda wa kumanne buta  
 ta pedha ya kumanne kiatu litigine hinyo  
 kufanya singhuli za lejani kuskoq  
 katika utengeneraji wavyatu kuna  
 gharana mbalimbali sinato za rifa'a nya  
 kufanya materi pengetahuan ya matu. Zifata  
 zo miatus za lajuata katika kudanira  
 gharana yang'cia nya materi pengetahuan ya matu  
 katiani rifa'a viaranya litajika katika  
 utengeneraji wa matu. Utengeneraji wa matu  
 anapawa kubaini rifa'a viaranya litajika katika  
 kasi yate.

" Kubaini upatkanaji wate. Utengene  
raji wa viatu anapaswa kubaini kwa vifaa  
hivyo ni nayo litajika niawere kufakata  
wapi kwa urahisi. Hii mamwesha mte  
ngeneraji wa viatu kupata diri ya upatkanaji  
wa vifaa."

Kubaini gharama kwa kila kifaa  
linacho litajilca. Hii itamwesha mte  
meraji wa viatu kuwere kufadilia gharama  
ya jumla ya vifaa nyote na posa aliyo.

11 nayo

Kufadilia gharama ya vifaa, katika  
hatua hii utengenearaji wa viatu ati  
kadiria vifaa vifaa atakanyo nuna kitokan  
ana posa aliyo nayo.

Utengenearaji wa viatu unanunuli  
mumkubwa kwa viatu kwani huuwe  
zisha viatu kujapitia kipata

